SOMO LA TANO



KWA NINI KIFO CHA YESU NI CHA THAMANI?

Tafadhali andika jina lako hapo juu kisha jaza nukuu za Biblia katika nafasi zilizotolewa.

YESU ALIONWA NA MASHAHIDI WENGI

Jiwe/kifuniko cha kaburi kwa tukio lililopita

Historia ilitokea – na matukio mengi ya kale, kama nguzo za Misri zlilibakia kuyadhibitisha. Walibeba ushahidi wa matukio yaliyotokea kwa miaka mamia iliyopita. Kufufuka kwa Yesu pia kulitokea, lakini hakuna kilichobakia kwa sababu kaburi lilikuwa tupu! Badala yake tuna kitu zaidi cha kushawishi – mwandishi aliandika juu ya wale waliomwona akiwa hai baada ya kifo Chake.

Maisha, miujiza, na kufufuka kwa Yesu, waandishi wa Agano Jipya wanasema, siyo kwamba ni hadithi za kielimu/ujanja zilizoandikwa,[1] ila ushahidi wa macho unaoelezea hakika ya kilichotokea.[2] Kufufuka kwake kuna kiini katika mahubiri ya Kanisa la Kwanza[3] hivyo nasi tena lazima tusikilize ushahidi na kutoa uamuzi wetu.

YESU ALIONWA DHAHIRI NA WENGI

Kumbukumbu ya kihistoria:
Matajiri walizikwa ndani ya pango kama kaburi Kukiwepo jiwe mbele yake. Yesu "alikopa" kaburi la tajiri.

Tunaambiwa kuwa Yesu alikuwa hai siku ya tatu baada ya kusulubiwa Kwake, na kwamba alionekana wazi kwa wengi wakati wa kipindi kilichodumu siku arobaini. Angalia Matendo 1:3

.....

.....

.....

.....

MASHAHIDI WENGI WANAUFANYA UKWELI UDHIBITIKE DHAHIRI

Mashahidi wengi kuliko ilivyohitajika!

Mashahidi wawili au watatu walikuwa wanatosha kuthibitisha ukweli na kugundua mkosaji kulingana na sheria za Wayahudi[4]. Angalia idadi ya mashahidi waliohitajika kuthibitisha na kugundua ukweli wa kufufuka kwa Yesu! Soma 1 Wakorintho 15:3-9. Andika mistari hii 7-8

.....

.....

.....

[1] 2 Petro 1:16
[2] Luka 1:14
[3] Matendo 4:33
[4] Waebrania 10:28

ALIKUWA MTU HALISI – SIYO ROHO

Yesu alikula chakula kiasi

Wanafunzi walikuwa wakimwona Yesu kwa karibu. Hakuwa mbali na kuona kivuli, wala hakuwa roho. Kuwashawishi na kuwahakikishia, Yesu aliwaonyesha makovu ya mikono na miguu yake iliyotobolewa na kuwasihi wamguse. Pia alikula chakula kilichopikwa ili kuthihisha kuwa mwili Wake ulikuwa sahihi.[5] Angalia Luka 24:39

.....

.....

.....

Hawakuweza kutoa mwili

WANAFUNZI HAWAKUPENDA KUDANGANYA

Yesu alikuwa na maadui wengi. Waliohusika na kifo chake walisema hakufufuka. Hata hivyo, hawakuweza kuutoa kaburini mwili wa Yesu ili kuthibitisha kuwa bado ni maiti. Hivyo walisambaza habari za uongo kuwa wanafunzi waliuiba mwili na wakawa wanadanganya juu ya ufufuko wake.[6] Lakini haiaminiki kama wanafunzi wangebuni ufufuko wa Yesu kwa sababu zifuatazo:

UONGO UNAKATALIWA KATIKA INJILI ZOTE KWA KIWANGO CHA JUU

Waandishi wa Agano Jipya wanawataka waumini kuishi maisha ya kiwango cha juu kama alivyoishi Yesu Kristo. Kuupinga uongo kwa wanafunzi kuliuonyesha kuwa watu waaminifu na wakweli.

Angalia Waefeso 4:25

Watu imara waaminifu

.....

.....

.....

Ni dhambi kudanganya, lakini pia ni vibaya zaidi kushawishi waumini wengine kuuamini uongo wako. Wanafunzi walihubiri wenyewe ufufuko wa Yesu kuwa ni kweli na unapaswe kuaminiwa.[7]

KUSINGEPATIKANA FAIDA YOYOTE KWA KUDANGANYA

Hakuna faida yoyote, mauti tu.

Watu wanapodanganya wanategemea kupata kitu, au wanaweza kusema ukweli pia. Mitume wasingepata chochote kutokana na kuongopa juu ya ufufuko wa Yesu, jinsi mamlaka yalivyokuwa yanachukia kutajwa kwa neon hili. Mitume walipoendelea kuhubiri kuwa Yesu alikuwa hai walichukizwa na kufungwa na *kifo*. Soma Matendo 5:30-33.

Andika mstari wa 30 na 33

.....

.....

.....

.....

[5] Luka 24:41-43

[6] Mathayo 28:12-13

[7] Linganisha 1 Wakorintho 15:14-15

WANAFUNZI HAWAKUWA WEPESI KUDANGANYIKA

Baadhi ya watu wanasema kuwa wanafunzi walikuwa waaminifu na watiifu ambao kwa wepesi walifikiri kama wamemwona Yesu. Kwa maneno mengine, walikuwa wamedanganyika kimawazo kuwa amefufuka. Lakini kuna sabafu za msingi kwa nini kufufuka ni mbali na kufikiri. Linganisha yanayofuata:

Chakula cha asubuhi na Yesu

KUONEKANA MCHANA KUNAONYESHA KUWA HAIKUWA KUFIKIRI

Ni mara chache mawazo kufikiri vitu visivyokuwepo kwa upana mchana kweupe. Yesu aliojionyesha mchana katika matukio tofauti tofauti. Tukio mojawapo ni lile wanafunzi walipokula pamoja nao asubuhi mwaloni! Soma Yohana 21:1-14. Andika mstari wa 12

.....

.....

Fikra?

.....

.....

HAIWEZEKANI KUWA WENGI WALIDANGANYIKA

Linganisha tena watu wengi ambao walimwona Yeshu hai. Tukio moja watu 500 walikuwepo. Je! Wote hawa walidanganyika? Angalia 1 Wakorintho 15:6

.....

.....

Mia tano walimwona kwa mara moja

.....

.....

BAADAYE MATESO YANGEKUWA HALALI KUHAKIKI

Wale wanaodanganya kwa fikra/hisia za porini/jangwani hugubikwa na mawazo yanayoumiza wanapopingwa. Hatari ya kifo humpelekea mtu “chini arthini”. Wanafunzi hawakuteseka kutokana na kuendelea kwa fikra. Kwa hakika walihakikisha kuwa Yesu yu hai, na walikuwa tayari kufa kwa ajili ya hili. Angalia Matendo 7:59

.....

.....

Kwa nini kuteseka kwa ajili ya uongo?

.....

Wengi katika Yerusalemu walihakikishiwa kuwa Yesu alifufuliwa kutoka mauti. Walikuwa karibu na tukio na wangeweza kuchunguza habari hii wao wenyewe kwa uhakika kabla ya kukutana na upinzani na hatari katika maisha yao. Walikuwa wakiandaliwa kuteseka kwa ajili ya ukweli, lakini siyo kwa ajili ya uongo au uzoefu wa fikra.

Baada ya adhabu huja faraja

UFUFUKO ULIKUWA UNATARAJIWA

Tunatakiwa kutegemea kufufuliwa kwa Yesu kutoka mauti kama aliteswa kwa ajili yaw engine. Kwa ajili ya fidia ya dhambi kulipwa, hakukuwepo na sababu zaidi za mauti kumshikilia. Si halali kuendelea kumfunga mfungwa zaidi endapo amemaliza hatia yake!

KAMA YESU ALIIFIA DHAMBI ILIMPASA KUFUFUKA

Kama Yesu hakufufuka, hakuna sababu ya kuamini kwamba adhabu aliyoipata ilikuwa inatosha. Muumini angebakia na hatia ya dhambi na angekosa nafasi Mbinguni. Angalia 1 Wakorintho 15:17

.....

.....

Kwa hiyo, kufufuka kwa Yesu ni kwa muhimu kwa mwenye dhambi ili atanganzwe kuwa anakubaliwa na Mungu.[8]

Muumbaji hawezi kufa!

KAMA MWANZILISHI WA UHAI, YESU ALIPASWA KUFUFUKA

Kama Yesu ni Mungu (somo la 1) haiwezekani mauti kumshinda. Aliyetoa uhai kwa kila kitu,[9] hawezi kushindwa na mauti.
Angalia Matendo 2:24

.....

.....

.....

ILI KUTOA MAISHA YA BAADAYE, YESU ALIPASWA KUFUFUKA

Yesu alifufuliwa kama mfano wa jinsi wengine watakavyofufuliwa atakapokuja duniani. Yesu alilipa garama ya dhambi ili kwamba matokeo yote ya dhambi yaweze kufutwa. Hii ni pamoja na kifo cha mwili. Waamini watakishinda kifo, kama vile Yesu alivyoshinda. Atakaporudi miili yao itafufuliwa kuwa hai tena.[10]

Yesu wa kwanza kwa wengi

NA MWISHO

Yesu alipaswa kuwa hai la sivyo asingeweza kusimama kuwa hakimu wa ulimwengu. Ufufuko ulikuwa ishara thabiti kuwa Yesu hakika atakuwa hakimu wa ulimwengu.[11]

Kulingana na ulinganifu huu, msimamo wako ni upi juu ya kufufuka kwa Kristo? Matukio yaliyolinganishwa hapa ni makubwa, na mada ni muhimu sana, kwamba unahitaji uamuzi.

[8] Warumi 4:25
[9] Matendo 3:14-15
[10] 1 Wakorintho 15:22-23
[11] Matendo 17:31